

**JE, YAWEZEKANA
KUISHI
BILA KUTENDA DHAMBI?**

JOE CREWS

**JE, YAWEZEKANA
KUISHI
BILA KUTENDA DHAMBI?**

Na Joe Crews

(Hotuba Na. 16 ya Mambo ya Kweli Yanayoshangaza)

Mfasiri: M. Mwamalumbili

Is It Possible To Live Without Sinning? - Kiswahili

JE, YAWEZEKANA KUISHI BILA KUTENDA DHAMBI?

Hivi karibuni nilisoma kisa kimoja cha kushangaza sana cha mtu aliyekubali kufanyiwa jaribio la kisayansi la hiponosi (hypnosis) [kiinimacho]. Akiwa chini ya ushawishi mwepesi wa kumzubaisha kutokana na kiinimacho kile alipewa amri ya kuinyanyua gilasi iliyokuwa mezani. Japo yeye alikuwa na nguvu nyingi, mwenye umbo shupavu la mwili, mtu yule hakuweza kuisogeza gilasi ile kutoka mahali pale ilipokuwapo. Jitihada zake alizofanya kwa nguvu zake zote hazikumwezesha kuinyanyua gilasi ile iliyokuwa nyepesi kiasi cha kutosha kwa mtoto mchanga awaye yote kuiondoa pale.

Kwa nini hakuweza kufanya vile? Kwa sababu wanasayansi wale, baada ya kumweka katika hali nzito ya usingizi wa kumduwaza, walikuwa wamemwambia kwamba ilikuwa haiwezekani kabisa kwake kuinyanyua gilasi ile. Kwa sababu akili yake ilisadikishwa kwamba isingewezekana kabisa kwake kufanya vile, mwili wake ulikuwa hauwezi kutekeleza amri ile ya kuinyanyua gilasi ile. Hayo ni maonyesho ya kuisimua jinsi gani yanayoonyesha kwamba hakuna mtu awaye yote anayeweza kutii kweli kweli amri anazoamini kwamba haziwezi kutekelezwa kabisa!

Je, hivi ndiyo maana Wakristo wengi wanaishi maisha yaliyo dhaifu, ya kushindwa-shindwa tu? Hapana shaka kwamba theolojia ya kisasa inayopendwa sana na watu wengi imekuwa ikiwafundisha mamilioni ya watu kwamba hakuna mtu ye yote anayeweza kuishi kweli kweli bila kutenda dhambi. Amri zile Kumi zimeonyeshwa nao kuwa ni kanuni ya maadili [tabia] inayofaa ambayo iliwekwa kwa kusudi tu la kuwafanya watu watambue haja yao.

Wakristo wengi wa siku hizi wanaugeukia zaidi na zaidi msimamo ule ulio laini, unaodekeza, kuhusu somo hili la kuishika Sheria [Amri Kumi]. Wao wanaamini kwamba upendo wa Mungu haupatani kabisa na sheria kali pamoja na adhabu zake zinazoambatana na uvunjaji wa sheria hizo.

Hilo ni fundisho linaloliwaza [linalotuliza moyo] sana, lakini ni geni kabisa na kile ambacho Biblia inafundisha. Mamilioni wanawekwa katika mazoea (conditioned) ya kuivunja ile Sheria Kuu ya Maadili [Amri Kumi] inayoyafunga malimwengu yote - bila kujisikia kwamba wanayo hatia! Neno la Mungu halimpi mtu ye yote udhuru wa kujisikia kwamba ana raha katika dhambi. Ni tatizo kuu la kila mtu aliyepata kuzaliwa hapa. Kama ugonjwa ule unaoambukiza sana, kila mtu ameambukizwa na dhambi hiyo na kuingiwa na vidudu vibaya vya magonjwa [virusi] vinavyoleta mauti, wala hakuna tiba yo yote iliyoapatikana katika dunia hii au kinga yo yote ili kuweza kuuzuia ugonjwa huo wa kufisha usiendele kuenea.

Tangu dhambi ilipoonekana kwa mara ya kwanza katika Bustani ile ya Edeni imekivuruga kabisa kila kitu kilichokuwa kizuri. Hakuna hata mara moja ilipopata kuishi bega kwa bega na haki na utakatifu. Matakwa ya Mungu hufanya isiwezekane kabisa kwa dhambi au uasi [uvunjaji wa Amri Kumi – 1 Yoh. 3:4, AJKK] kuwa sehemu ya mtindo wa maisha ya Mkristo. Hali mpya iliyopo ya kuivumilia dhambi si ya Kibiblia kwa maana ıwayo yote ya neno hilo. Yesu alikuja kuwaokoa watu kutoka katika hiyo dhambi. Haitaingia kamwe Mbinguni. Mtazamo wetu kuhusiana nayo hauna budi kuwa ule wa kutoafikiana nayo. Hapawezi kuwapo na hoja ya kuifanya dhambi ipate kukubalika zaidi kwa kupunguza ukubwa wake au kwa kuigeuza sura yake. **NI LAZIMA IANGAMIZWE KABISA.** Na njia peke yake ya kuiondolea mbali ni kuwa kuupokea utimilifu wa Yesu Kristo pamoja na neema yake katika maisha yetu.

Ni jambo la ajabu jinsi gani kwamba washiriki wa kanisa wengi sana hivi sasa wamegeuka, wanaitetea dhambi kana kwamba haiwezi kuzuiwa isipate ushindi wo wote katika maisha ya Mkristo.

Hivi tunawezaje kuthubutu kuueleza vibaya uwezo wa neema ya Mungu unaopatikana katika Injili! Yesu tayari amemshinda Ibilisi, na Mkristo ye yote yule asingeweza kutishwa na adui huyo aliye duni kabisa, yaani, aliyeshindwa. Sisi hatuna shughuli yo yote ya kufanya ili kuutetea *uvunjaji wa Amri Kumi*.

Ni jambo zito la kutosha kujishughulisha kwa makusudi katika tendo lo lote la dhambi [uvunjaji wa Amri Kumi], lakini ni jambo la kufisha kabisa kuitetea dhambi [uvunjaji wa Amri Kumi] kama kitu kisichoweza kuzuiwa. Kusema kwamba ushindi hauwezekani kabisa ni kukana utoshelevu wa injili, na kukanusha sehemu kubwa ya Maandiko yaliyovuviwa. Zaidi ya hayo, jambo hilo linaunga mkono shtaka la kwanza la Shetani dhidi ya Mungu, na kumpa kila mmoja anayeliadini usalama wa bandia, unaopumbaza akili.

Mara nyingi watu wanaitetea dhambi kwa sababu, kwa kutegemea nguvu zao wenyewe, wao hawajaweza kuacha kuifanya. Kwa mfano, wasipoweza kuacha kuvuta tumbako, basi, wao hulazimika kutafuta sababu ya kuwamo dhambi katika maisha yao kwa kutumia akili zao za kibinadamu. Badala ya kufanya ungamo linalowashusha hadhi yao kwa kukiri kwamba hawawezi kuishinda [kwa nguvu zao], wao wanatunga sababu za uongo wakisema kwamba kwa kweli dhambi hiyo haiwaletei madhara yo yote au kwamba hakuna awezaye kuwa mkamilifu. Au wanafuata fundisho lile linalopendwa sana na watu wengi, ambalo linawafaa wao, lisemalo kwamba kwa vyo vyote vile hakuna mwanadamu ye yote awezaye kuishi kikweli kweli bila kutenda dhambi.

Pengine ni salama kusema kwamba Wakristo wengi sana siku hizi wamesalimu amri kwa kuyakubali matokeo ya maisha yao ya kushindwa katika kuitimiza Sheria hiyo ya Maadili [Amri Kumi]. Kwa kweli, wao wanaridhika sana na wazo kwamba Mungu hawatazamii wao kuitimiza Sheria hiyo [Amri Kumi] kabisa kabisa katika mwili wao huu au katika roho zao. Matokeo ya mafundisho kama hayo ni kama vile mtu ambavyo angeweza kutarajia - wapo watu wengi wasiokuwa na furaha moyoni, lakini ambao ni washiriki waasi [wavunjaji wa Amri Kumi] wa kanisa, waona kwamba kuwa na wasiwasi wo wote juu ya kuzishika amri hizo [kumi] ni kama kuchagua utitiri, tena ni njia ya kujipatia wokovu.

Ni mkakati gani huo wa udanganyifu utokao kwa yule Shetani! Akiwa ndiye mbunifu wa fundisho hilo, Ibilisi analiunga mkono tu lile shtaka lake la zamani lisemalo kwamba Mungu alikuwa anataka mambo mengi mno. Alimshtaki Mungu kwamba alikuwa hana haki kudai kitu fulani kilichokuwa hakiwezekani [toka kwa viumbe vyake]. Alifanikiwa kuwashawishi theluthi moja ya malaika kwa kuwaambia kwamba Mungu alikuwa hana haki kutazamia utii wao kwa Sheria yake [Amri Kumi – Yn. 8:44; 1 Yoh. 3:8,10], naye tangu wakati ule amekuwa akifanya jitihada yake kubwa ili kumfanya kila mtu apate kusadiki hivyo. Hebu na ulitafakari hilo kwa dakika moja hivi, utaona kwamba mpango huo mzima utaanza kuleta kwako maana zake nyingi za kishetani. Shetani anajua kwamba dhambi [uvunjaji wa Amri Kumi] ndicho kitu peke yake kitakachomzuia mtu awaye yote kuingia mbinguni. Kwa maana DHAMBI NI “UVUNJAJI WA SHERIA [AMRI KUMI]” (1 Yohana 3:4, AJKK; linganisha na Yak. 2:10-12), basi, ikamlazimu yeye kuukamilisha mpango wake kwa kuwafanya wanadamu walione kwa ni jambo rahisi tu kuivunja hiyo Sheria [Amri Kumi], na pia kuifanya ionekane kuwa ni ya kuchukiza mno [Ufu. 12:17]. Kulifanya wazo lake hilo lipate kukubaliwa na Wakristo, Shetani aliweza kulifanya kwa siri ili liwe fundisho na kulingiza kwa hila katika Ukristo ule wa maridhiano [uliopata na upagani].

Katika kila mkutano mkuu wa mahubiri ya Injili, tunakutana nalo katika sura moja au nyingine, kwa kawaida tunapolifikia somo lile la Sheria [Amri Kumi] na Sabato. Madai ya utii yanayowakosesha raha yanakataliwa na watu kwa kuinua juu mabega yao kwa dharau na kusema, “Sawa! kwa vyo vyote vile hakuna anayeweza kuzishika hizo Amri Kumi.”

Lakini tatizo hilo haliishii hapo. Hata na Wakristo wale waliokwisha kuyakubali madai ya Sheria hiyo ya Maadili [Amri Kumi] hawajali sana kama wanaitekeleza vizuri ipasavyo. Kwa njia ambayo ni vigumu kufahamu, wao wameathiriwa na imani iliyopo isemayo kwamba kuwa na wasiwasi sana juu ya utii ni aina fulani ya wokovu kwa njia ya matendo. Kwa namna ya kushangaza, wengine wanaonekana kana kwamba wanaogopa sana kuishika hiyo Sheria [Amri Kumi] kwa makini sana kiasi kwamba wanauacha kabisa mwanya wa kuivunja. Kwa kufanya hivyo wanajifariji wenyewe kwa mawazo yao potofu kwamba wao hawaishiki Sheria hiyo [Amri Kumi] kwa lengo la kujipatia wokovu.

Je, watu hao waliojitoa kuzishika amri [kumi] za Mungu wanawezaje kuifikia hali hiyo ya kuchanganyikiwa vibaya inayojikanusha yenyewe ndani yao? Kupokea dhana [mawazo] potofu ya wokovu kwa imani ni sehemu tu ya jibu lake. Sehemu kubwa ya tatizo hilo imejengwa juu ya kushindwa kwao wanadamu na udhaifu wao wa mwili. Kwa kuwa walijikuta wanajikwaa wenyewe katika juhudi zao za kutaka kuwa wakamilifu, basi, mwishowe waliamua kwamba ilikuwa haiwezekani kabisa kutokutenda dhambi. Kutoka mahali hapo ilikuwa ni rahisi kuanza kuyatafsiri mafungu ya Biblia ili kutetea udhaifu wao walio nao katika maisha yao. Shetani alitumia kwa manufaa yake mwelekeo wa kisaikolojia wa akili ya kibinadamu wa kutafuta sababu za kutetea kosa, na mara hiyo wakawa wamelivumbua fundisho lililowapa faraja, ambalo liliruhusu kuwapo kwa upotovu wao huo wa kutoifuata Sheria hiyo [Amri Kumi] mara kwa mara. Kwa sababu hiyo, Wakristo wengi mno hivi leo wamejidekeza [wamejiachia] kuwa na maisha yanayobadilikabadilika tu ya KUSHINDA-KUSHINDWA, KUSHINDA-KUSHINDWA. Kwao huo ndio mtindo uliokubalika wa maisha ya kawaida ya Ukristo wao.

Lakini kwa namna ya kutia hofu kuna kitu fulani kisichokuwa sawa kuhusu msimamo wao huo. Kwanza kabisa, fundisho lo lote la dini lisijengwe kamwe juu ya msingi wa hisia [mawazo] au uzoefu wa maisha ya kibinadamu. Ni lazima liwe na mizizi yake katika mafundisho yanayoeleweka wazi, yasiyo na maana mbili au zaidi ambayo yanatoka katika Neno la Mungu. Ni kweli kwamba mafungu ya Biblia yanaweza kukusanywa pamoja ambayo yanaonekana kwamba yanaliunga mkono fundisho hilo lisemalo kwamba mwanadamu hawezi kuwa na ukamilifu wo wote wa kiroho. Tunahakikishiwa ya kwamba wote wamefanya dhambi [Rom. 3:23], kwamba nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu [Rum. 8:7], na ya kwamba haki ya mwanadamu ni kama nguo iliyotiwa unajisi [Isa. 64:6]. Lakini mafungu yote yanayohusu kushindwa, dhambi, na kuzidiwa nguvu yanahusu maisha ya mtu ambaye HAJAZALIWA MARA YA PILI. Kuna mafungu mengine mengi yenye maana iliyo wazi ambayo yanaonyesha kwamba upo uzoefu wa kupata ushindi kamili na kuishi maisha ya Kikristo bila kutenda dhambi, kinyume na uzoefu ule mwingine [wa kushinda-kushindwa, kushinda-kushindwa]. Katika kila mfano uliotolewa yanahusu maisha ya mwana wa Mungu ALIYEONGOKA na kujazwa na Roho, yaani, mwana wa Mungu aliyejitoa kabisa kwa Mungu.

Tofauti hiyo ni lazima itambuliwe sikuzote katika usomaji wa Maandiko. Injili ya Yesu Kristo ni UWEZA wa Mungu uuletao wokovu. Neema yake ina nguvu kuliko mamlaka zote za uovu zikiunganishwa pamoja. Yesu alikuja kuwaokoa watu wake KUTOKA katika dhambi zao [sio kuwaokoa pamoja na dhambi zao]. Hakuna mtu ye yote anayesoma kwa akili sura ya sita ya Warumi awezaye kuamini kwamba Mkristo yuko huru kutenda dhambi. Paulo analivunjilia mbali kabisa fundisho hilo lisemalo kwamba muumini analazimika kuendelea daima kuanguka dhambini.

Ni kweli kwamba mpango wa kutakaswa umewekwa ENDAPO dhambi imetendwa [1 Yoh. 2:1,2; 1:7,9]; lakini mpango kamili wa Mungu ulifanya uwezekano uwepo kwa mwanadamu wa kuishinda kila dhambi na kuishi maisha yake ya UTII KAMILI [kwa zile Amri Kumi] kwa njia ya Kristo [Rum. 8:1-4; Flp. 4:13]. Kwa kweli, ahadi za Biblia ziko wazi mno na bayana juu ya jambo hilo hata ni vigumu kuchanganyikiwa. Hakuna maana ya siri [iliyojificha] au sharti lililojificha liwezalo kupatikana katika mafungu mengi sana yanayoelezea maisha ya ushindi ya mwana wa Mungu

aliyezaliwa mara ya pili. Na kwa kuwa mtu anaweza kuwa hajapata kukulia katika imani ile kamilifu ambayo inaleta ushindi unaoendelea daima, basi, asikane kwamba hakuna uwezo wa wote wa Mungu unaoweza kumpa ukombozi kama huo. Petro alipoanza kuzama katika ile Bahari ya Galilaya haikuwa kwa sababu Mpango wa Mungu au Uweza wake ulikuwa umeshindwa. Petro angeweza kutoa sababu kwa kutumia akili za kibinadamu, kama Wakristo wengi mno wa siku hizi wanavyofanya, na kusema, “Mungu hakutaka mimi nitembe juu ya maji, tena, zaidi ya hayo, kwa vyo vyote vile haiwezekani kabisa kwa mwanadamu ye yote kufanya kitu kama hicho.” Kama walivyofanya wazazi wetu wale wa kwanza, sisi bado tunaelekea kuiweka lawama ya mwisho juu ya Mungu tunaposhindwa kuufuata mpango wake wa kuishi maisha matakatifu.

Ushindi Kamili Umeahidiwa

Roho wa Mungu alionekana kana kwamba alikuwa anatazamia kuliona pambano lile ambalo wengi wangelipitia kwa kuzitegemea ahadi zile za Biblia kuwapa ushindi kamili. Kwa sababu hiyo waandishi waliovuviwa waliongozwa na Roho kutumia lugha inayoonekana kana kwamba inazidi mno katika kuelezea uwezekano wa kuishinda dhambi. Maneno yanayozidi kiasi yanatumika ambayo huyafanya mawazo yetu kuwa na mashaka mengi. Badala ya kusema kwamba tunaweza kuokolewa, Biblia inasema kwamba sisi tunaweza “KUOKO[LEWA] KABISA” (Waebrania 7:25). Badala ya kusema tunaweza kushinda, inatuhakikishia kwamba tunaweza kuwa “ZAIDI YA WASHINDI” (Warumi 8:37, KJV). Badala ya sisi kuambiwa kwamba tunaweza kustahili kushinda, tunaambiwa kwamba tunaweza “KUSHANGILIA [KUSHEREHEKEA] USHINDI DAIMA” (2 Kor. 2:14, KJV). Badala ya kutuahidi kwamba msaada wa wote tutakaoomba kwake ili upate kutusaidia katika vita zetu za kiroho, Biblia inatuambia kwamba yeye anatupa “MAMBO YA AJABU MNO kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo ...” (Waefeso 3:20). Na fungu lile lililo kabla tu ya hilo linatuhakikishia waziwazi kwamba sisi tunaweza ku“TIMILIKA KWA UTIMILIFU WOTE WA MUNGU” (fungu la 19).

Hakika, nyingi miongoni mwa ahadi hizo ni pana mno kwa akili zetu finyu za kibinadamu kuweza kuzielewa kikamilifu, lakini bila shaka zimekusudiwa kutugusa ili tupate kuona ukubwa wa nguvu za Mungu alizo nazo kwa ajili yetu. Kama lugha hiyo inaonekana kana kwamba imetiwa chumvi mno, basi, ni kwa sababu sisi tuna imani dhaifu mno, tena tumekuwa dhaifu kimwili kuweza kusadiki kwamba *usafi wa maisha kama huo pamoja na utakaso ungeweza kutimizwa ndani yetu*. Tunaelekea mno kuzitegemea hisia zetu kwa haraka sana kuliko Neno la Mungu.

Je, ni muhimu kwetu kuziamini kabisa ahadi hizo kama zinavyosomeka? Ndiyo, kwa sababu ni kwa njia ya ahadi hizo tu ukombozi wetu unaweza kupatikana. “Tena kwa hayo ametukirimia AHADI KUBWA MNO, ZA THAMANI, ili kwamba kwa hizo mpate kuwa WASHIRIKA WA TABIA YA UUNGU, mkiokolewa na uharibifu uliomo duniani kwa sababu ya tamaa.” 2 Petro 1:4.

Hebu zingatia kwamba ni “KWA HIZO” sisi tunaweza kuokolewa na [kutoka katika] uharibifu wa dhambi. “HIZO” ni nini? Ni ahadi za Mungu. Mfululizo wa ushindi umewekwa wazi katika fungu hilo la ajabu sana. Kwa njia ya imani katika ahadi hizo sisi tunakuwa washirika wa tabia ya Uungu, na kwa nguvu ya tabia hiyo mpya ndani yetu sisi tunaweza kuokolewa [kuepukana] na uharibifu wa dhambi. Kwa maneno mengine, kila kitu hutegemea juu ya kujisalimisha nafsi yako na kujitua ili Roho wa Kristo apate kukaa ndani yako. “PASIPO MIMI,” Yesu alisema, “ninyi HAMWEZI kufanya neno lo lote.” Yohana 15:5.

Fungu la maana lililo sawa na hilo ni maneno ya Paulo yaliyovuviwa, yasemayo, “Nayaweza MAMBO YOTE katika yeye anitiaye nguvu.” Wafilipi 4:13. Usemi huo mdogo “mambo yote” ndio UFUNGUO WA USHINDI kwa kila mmoja wetu. Unajumuisha uwezo juu ya madawa ya kulevya,

uasherati, ulafi, kiburi, na kila tendo la dhambi ambalo lingeweza kutunyang'anya sisi uzima wa milele.

Mambo Yote Tunayo

Jambo kubwa hapa ni kwamba unapoupata uweza wa Kristo katika maisha yako, basi, unapata kila kitu ambacho ungeweza kukitamani. “Yeye aisiyemwachilia Mwana wake mwenyewe, bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote, atakosaje kutukirimia na MAMBO YOTE pamoja naye?” Warumi 8:32. Hapo tena tunaupata usemi ule ule - “mambo yote.” Pia utaupata katika 2 Petro 1:3: “Kwa kuwa uweza wake wa Uungu umetukirimia VITU VYOTE vipasavyo [MAMBO YOTE YAPASAYO] uzima na utauwa...”

Unapoyaweka mafungu hayo pamoja picha ambayo ni vigumu kuamini inajitokeza. Kule kudai kwamba Kristo yuko katika maisha yako, kunakufanya upokee pia kila kitu alichochacho Kristo. Paulo anatoa ufafanuzi wake kwa njia hii: “Bali kwa yeye ninyi mmepata kuwa katika Kristo Yesu, aliyefanywa kwetu hekima itokayo kwa Mungu, na haki, na utakatifu, na ukombozi.” 1 Wakorintho 1:30.

Hapo “mambo yote” yamegawanywa katika uzoefu maalum wa maisha ya kila mtu, nasi tunaanza kuona kwamba Petro alikuwa na haki kusema kwamba Mungu ametupa vitu vyote vipasavyo utauwa. Wakristo wale wanaouonea mashaka uwezekano wa kuzishinda dhambi kabisa ingewapasa kuyasoma mafungu hayo kwa makini. Je, maneno haya “haki,” “ukombozi,” na “utakatifu” yanajumuisha nini? Yote matatu katika maneno hayo yanatuhidi sisi zaidi ya ukombozi ule wa kutoka katika hatia ya dhambi zetu zilizopita. Neno hili “ukombozi” halijafungwa kuhusiana tu na ukombozi kutoka katika hatia ya dhambi, bali pia kutoka katika uwezo wa dhambi. “Utakatifu” ni neno linaloelezea ukuaji unaoendelea, unaokua kila siku katika kuishinda dhambi. “Haki” kwa maana yake inayoeleweka wazi ni kutenda haki, nalo hutumiwa wakati nguvu ya kutimiza mapenzi ya Mungu inapoleta matokeo hayo. Hayo yote ni maneno makubwa sana, lakini yote kwa maana ile nyingine yanamaanisha kuwekwa huru kutoka katika hatia ya dhambi pamoja na utendaji wa dhambi.

Kila mwana wa Adamu anahitaji vibaya sana mambo mawili - MSAMAHA kwa wakati uliopita, na UWEZO kwa ajili ya siku za usoni. Ukombozi unajumuisha yote mawili; na wazo lile lisemalo kwamba wokovu KAMILI kutoka katika hatia ya dhambi unahusika, lakini kwamba ni kwa SEHEMU tu tumepewa wokovu kutoka katika uwezo wa dhambi, ni upotoshaji wa injili. Yesu hakuja kutuokoa sisi kutokana na matokeo ya dhambi tu, bali kutuokoa sisi mbali na dhambi yenyewe. Wokovu si kitu cha kukana tu; si upungufu wa [kutokuwapo kwa] kitu fulani tu. Yeye hakuja kwa madhumuni ya kukiondoa kitu fulani tu - yaani, hatia yetu ya dhambi, bali kutupa sisi kitu fulani - yaani, USHINDI JUU YA DHAMBI. Kwa upande wa Mungu kule kutusamehe sisi na kutuacha chini ya uwezo wa dhambi inayoendelea lingekuwa ni tendo la kumfanya Mungu kuwa mshirika katika maovu hayo. Yeye *hatuhesabu* sisi kuwa tu wenye haki tu kwa kutuhesabia kifo chake kinachotupatanisha naye, bali yeye *anatufanya* sisi kuwa wenye haki kwa KUTUGAWIA MAISHA YAKE YA USHINDI ili yawe sehemu halisi ya maisha yetu.

Baada ya kusoma kwa makini sura yote ya sita ya Warumi, kama unahitaji uthibitisho zaidi unaweza kuupata, hebu soma:

1 Wakorintho 15:57 - “Lakini Mungu na ashukuriwe ATUPAYE KUSHINDA kwa Bwana wetu Yesu Kristo.”

1 Yohana 5:4 - “Kwa maana kila kitu kilichozaliwa na Mungu HUUSHINDA ULIMWENGU; na huku ndiko kushinda kuushindako ulimwengu, hiyo IMANI yetu.”

Wafilipi 2:5 - “IWENI NA NIA IYO HIYO ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu.”

2 Wakorintho 5:21 - “... ili sisi TUPATE KUWA HAKI ya Mungu katika Yeye.”

1 Yohana 3:6 - “Kila akaaye ndani yake HATENDI DHAMBI; kila atendaye dhambi hakumwona yeye, wala hakumtambua.”

Hebu kwa dakika moja hivi tuurudie ule mfano wa mtu yule aliyetiwa katika hali ya usingizi upumbazao ili kumfanya atende mambo anayoamriwa kutenda. Hakuweza kuinua juu gilasi ndogo toka mezani kwa sababu mawazo yake yalikuwa yamesadiki kabisa kwamba jambo lile lisingewezekana kulifanya. Je, hivi Shetani ameweza kulifanya kanisa lishindwe kusonga mbele kwa kutumia uwezo huo wa uongo wa kulilaza usingizi na kuliambia kwamba utii hauwezekani kabisa? Ni hakika kwamba mambo hayo yanaonekana kuwa hivyo.

Hakuna mtu ye yote awezaye kutumia jitihada yake yote kufanya jambo fulani analoamini kwamba haliwezekani kabisa kwake. Basi ni wazi kwamba wale wanaoamini kwamba hawawezi kuishi bila kutenda dhambi, hawajitahidi kuishi bila kutenda dhambi. Hakuna mtu mwenye akili awaye yote ambaye atapoteza muda wake na juhudi yake yote kutekeleza jambo lile ajualo kwamba juhudi yake itakuwa ni bure kabisa.

Jambo hilo linatufikisha sisi kwenye swali la kuvutia sana: Je, mtu anaweza kuamini kwamba hakuna njia yo yote ya kuacha kutenda dhambi, na wakati uo huo kufanya mpango wa kuacha kutenda dhambi? Kimantiki, jambo hilo lingeonekana kwamba halielekei sana kutendeka, kama si vigumu kabisa kulitenda. Walakini Biblia inatuagiza sisi kwamba tu“SIUANGALIE MWILI, HATA KUWASHA TAMAA ZAKE.” Warumi 13:14. Je, hivi ni kweli kwamba tunafanya mpango wa kutenda dhambi kwa kuendelea kwetu kulishikilia wazo lisemalo kwamba haiwezekani kabisa kutotenda dhambi?

Yeye Ashindaye

Kitabu chote cha Ufunuo kimeandikwa kwa makanisa saba ya Asia. Katika kila moja la makanisa hayo watu fulani walipata sifa nyingi sana na ahadi tukufu za kupewa thawabu mbinguni. Bila kubagua baraka ilitolewa kwa “yeye ASHINDAYE.” Makanisa yale saba ni mfano wa kila kipindi cha Kanisa la Kikristo kuanzia kipindi cha Mitume mpaka mwisho wa wakati. Ikiwa ushindi dhidi ya dhambi ni jambo lisilowezeke kabisa, basi, hakuna mtu ye yote ambaye ataokolewa katika karne zile zote za wakati.

Kukana kuwapo kwa uwezekano wa kupata ushindi kamili dhidi ya dhambi ni kumrubuni Mungu utukufu wa utume wake. Alikuwa, Biblia inasema, kuzivunjilia mbali kazi za Ibilisi. Kazi hizo ni matendo ya dhambi. Endapo hakuna mtu ye yote aliyedai uweza wake ili kuzishinda dhambi kabisa, basi, mashtaka ya Shetani yangukuwa yamethibitishwa. Matakwa ya Mungu [Amri Kumi] yangeonekana wazi kuwa ni magumu mno kuweza kuyatii.

Yesu alieleza kwamba alikuwa amekuja “ kutafuta na kuokoa kile kilichopotea.” Luka 19:10. Hapa yeye alidokeza kwamba yalikuwapo mambo mengine zaidi yaliyopaswa kurejeshwa pamoja na wanadamu. “Kile kilichopotea” kilijumuisha ile TABIA ISIYO NA DHAMBI. Utume wake ulikuwa ni kupinga na kuvunjilia mbali mpango mzima wa kuwanajisi wanadamu kwa dhambi aliokuwa ameuanzisha Shetani. Kuirejesha sura ya Mungu ndani ya mwanadamu ni sehemu ya maana sana ya ile Injili ya Milele [Ufu. 14:6,7]. Kazi hiyo ya Injili [ya kuwarudishia wanadamu tabia isiyo na dhambi] ni lazima ifanyike kabla Yesu hajaja, wala hilo si kama wazo fulani la kimwujiza lililotolewa baadaye na Bwana wetu anayerudi.

Kitabu cha Ufunuo kinaitambulisha tabia hiyo kamilifu ya wale waliokombolewa kuwa ni UTII [kwa zile Amri Kumi]. “Hapa ndipo penye subira ya WATAKATIFU, hao WAZISHIKAO AMRI [KUMI] ZA MUNGU na IMANI [MAFUNDISHO YOTE – Efe. 4:5; Mt. 28:19,20] YA YESU.” Ufunuo 14:12. “Joka [Shetani] akamkasirikia yule mwanamke [kanisa la kweli], akaenda zake afanye vita juu ya wazao wake waliosalia [waumini wake wa mwisho], WAZISHIKAO AMRI ZAKE [KUMI], na kuwa na USHUHUDA WA YESU [ROHO (KARAMA) YA UNABII - Ufu. 19:10].” Ufunuo 12:17. “Heri wale WAZISHIKAO AMRI ZAKE [KUMI], wawe na haki ya kuuendea huo mti wa uzima [Adamu alifukuzwa asiende kwenye mti wa uzima kwa uvunjaji wake wa Amri Kumi – Mwa. 2:22-24], na kuingia mjini kwa milango yake.” Ufunuo 22:14, Tafsiri ya toleo la King James.

Ni jambo la maana jinsi gani, basi, kwamba sharti lile alilopewa mwanadamu ili apate kuendelea kukaa Edeni pia ndilo sharti la kurejeshwa kwake katika Edeni. Mtu ye yote anayeamini kwamba utii hauna maana ingempasa kusoma tena kisa hicho cha kuisisimua cha Adamu na Hawa. Kosa lile dogo sana walilotenda kwa mwili wao lilileta msiba wote huu uliodumu kwa miaka 6,000 iliyopita [yaani, kuanzia Edeni hadi mwaka 2000]. Wale watakaorejeshwa katika Paradiso [Bustani ya Mungu/Edeni] ile iliyopotea watakuwa wameonyesha waziwazi kwamba wanaweza kuaminiwa kupewa uzima ule wa milele. Kwa njia ya uaminifu wao katika kutoa UTII wao mbele ya [wakiwa wamekabiliwa na] kifo, watakuwa wamethibitisha kwamba mashtaka ya Shetani ni ya uongo kabisa. Uaminifu wao thabiti utakuwa ndiyo dhamana yao ya uzima wa milele katika ufalme wa Mungu utakaokuwa umerejeshwa [hapa duniani – Dan. 7: 27,28].

Tuseme nini, basi, juu ya wale wanaoangalia matendo mema yanayotokana na huo utii [kwa zile Amri Kumi] kuwa ni jambo lisilo na maana? Hao ni watu waliodanganyika kabisa, tena wanacheza ndani ya mtego wa dhambi wa kufisha alioutega Shetani [2 Tim. 3:12-17]. Uzoefu wa maisha ulio bora kabisa wa wale walioongoka kweli kweli unauvunjilia mbali ule mtindo wa maisha unaotimiza tamaa mbaya za mwili bila kujizua pamoja na kutenda dhambi. Chini ya udhibiti wa Roho wa Mungu, mazoea mabaya ya mwili yanaweza kutawaliwa kabisa na kuondolewa katika maisha yetu. Kwa njia ya imani katika ahadi zake, uwezo, ambao ni vigumu kwetu kusadiki, unaweza kutolewa ndani ya maisha ya yule aliye tayari KUACHANA na anasa zake za dhambi.

Moyo wa Mungu unatamani sana kwamba sisi tumwamini yeye kama asemavyo katika neno lake, na tuweze kudai uwezo wake aliouahidi kutupa. Hiyo pekee ndiyo njia ya kufikia katika ushindi wa kweli. Lakini hakuna mtu ye yote awezaye kuuonja ushindi huo kama hasadiki kwamba ushindi huo unaweza kupatikana. Soma tena ahadi zilizomo katika Biblia. Usjaribu kuzipindisha ili zilingane na udhaifu wako na kushindwa kwako uliko nako katika maisha yako ya kibinadamu. **Zina maana ile ile kama zisemavyo.** Wokovu ni wako kwa kuamini na kuuomba.

Hapa yatupasa kutulia kidogo na kutafakari juu ya ukinzani ule unaoletwa sikuzote dhidi ya wale wanaoamini kwamba wanaweza kupata USHINDI KAMILI. Ukinzani huo unasema hivi: Kama wewe unaamini kwamba unaweza kuishi bila kutenda dhambi, je! unaweza kusema kwamba maisha yako hayana dhambi kabisa? Ingawa swali hilo linahitaji kupatiwa jibu, ni lazima ionyeshwe kwamba ukinzani huo hauna uhusiano wo wote na hoja yenyewe. Ikiwa Biblia imeuthibitisha ukweli fulani, basi, ukweli huo unapaswa kupokewa kwa misingi ya mamlaka ya neno hilo lililovuviwa, wala sio kwa msingi wa uzoefu wa maisha wa yule mjumbe. Ikiwa ushindi juu ya dhambi zote unawezekana kwa njia ya Kristo, basi, ushindi huo ni wa kweli, haidhuru kama mhubiri ameudai au hajaudai. Zaidi ya hayo, ile **kazi ya UTAKASO ni kazi inayoendelea daima, ni uzoefu wa maisha yote ya mtu,** wala hauwezi kufikiriwa kuwa umekamilika kwa wakati fulani wa baadaye [Flp. 3:12-15]. Hata kama mtu asingeweza kuitambua dhambi yo yote inayojulikana [katika maisha yake], asingeweza kujivuna na kusema kwamba hana dhambi [1 Yoh. 1:8-10]. Kusema kweli, mtu yule aliye karibu sana na ukamilifu kwa hakika angekuwa wa mwisho kabisa kuweza kutambua, kwa sababu kadiri

anavyokaribia zaidi na zaidi kwa Yesu, ndivyo kadiri atakavyojiona kwamba yeye si mkamilifu machoni pake mwenyewe.

Dai linaweza kutolewa pia kwamba fundisho hilo la ushindi juu ya dhambi ni wazo la hali ya juu sana kimaadili [kitabia], tena lina utata mwingi mno kitheolojia kuweza kuwekwa katika matendo ya mtu. Lakini basi, hakuna jambo lililo mbali sana na ukweli kama hilo. Hata mtoto mdogo anaweza kukielewa kitendo kile rahisi cha kuitumia imani yake katika kudai ahadi zile za Biblia. Hakuna zoea lo lote au dhambi yo yote ijulikanayo kwa mwanadamu ambayo haiwezi kudhibitiwa kwa njia ya imani.

Katika dakika chache zijazo utaweza kuona uzuri wa mpango huo wa Mungu wa ushindi. Utajifunza jinsi ya kuacha kuvuta sigara, kutukana, kula kupita kiasi, kusengenya, au kutenda dhambi nyingine yo yote. Usiruhusu jambo lo lote kuyageuzia kando mawazo yako wakati unaendelea kuisoma aya ifuatayo. Huenda kwako ikawa ndio mwanzo wa maisha mapya, yatakayokuwa ya thamani sana kuliko fedha yote iliyomo humu duniani. Kwa kuwa wengi wanapigana vita na sigara, mimi nitatumia zoea hilo baya kama kielelezo cha ushindi tunaoendelea kuuelezea humu. Weka tatizo lako katika fungu hilo, kisha chukua hatua hizo nne kuelekea kwenye ushindi mkubwa mno.

Siri ya Ushindi

Je, umepata kusikia habari za njia ya mageuzi yanayoendelea hatua kwa hatua ya kupata ushindi juu ya tumbako, au dhambi nyingineyo yote. Wakati mwingine inaitwa njia ya “KUPUNGUZA TARATIBU HADI KUWA NDOGO KAMA NCHA ILIYOCHONGOKA YA MSHUMAA,” lakini kwa kawaida njia hiyo haifanyi kazi yake barabara. Kwa kweli, inafanya kazi yake kwa sehemu tu kwa sababu UZEE unaondoa baadhi ya majaribu na dhambi, kisha WAKATI unayamaliza yaliyobaki kinapokuja kifo. Lakini, je, unajua kwa nini “KUJARIBU KUACHA” hakufanyi kazi katika kumshinda yule Mwovu?

Kwa nini tusipigane na yule mwovu kwa miezi michache na hatimaye kumfukuzilia mbali? Kwa kuwa yule mwovu anazo nguvu nyingi sana kuliko sisi. Tungeweza kupigana naye kwa mwaka mmoja, lakini bado yeye angeendelea kuwa na nguvu nyingi sana kuliko sisi mwishoni mwa mwaka ule. Kujaribu kuacha hakutaweza kamwe kuivunja nguvu ya dhambi hata kwa kuchukua mfano mmoja tu, kwa sababu tunamkabili adui ambaye daima atakuwa na nguvu nyingi sana kuliko sisi. Jibu ni lipi, basi, kwa udhaifu na kushindwa kwetu? Swali hilo linatufikisha kwenye siri nzuri na kuu sana ambayo imo katika Neno la Mungu. Hebu, basi, na tujifunze siri hiyo kwa makini na kwa maombi mengi.

Kwanza kabisa, ni lazima mtu ajue kwamba vipawa vyote vya Mbingu vinatolewa kwetu kwa njia ya ahadi zilizo katika Biblia, hizo tunazipokea kwa imani. Petro anaeleza juu ya “ahadi kubwa mno, za thamani,” kisha anatumia kamba “kwa hizo mpate kuwa washirika wa tabia ya Uungu.” 2 Petro 1:4. Nguvu nyingi sana imewekwa ndani ya kila ahadi ili ipate kujitimiza yenyewe kwa wale wote wanaoidai kwa imani. Ni wachache mno walio tayari kuamini kwamba baraka ile iliyoahidiwa **inakuwa yao wakati ule ule wanapoiamini** [Marko 11:24]. Mbona ni vigumu mno kuamini kabisa kwamba Mungu atafanya kile alichohidi kufanya?

Hebu sasa na tufike kwenye kiini chenyewe cha ushindi huo, na kutafakari hatua nne rahisi za Maandiko ambazo muumini ye yote anaweza kuzichukua anapodai kupewa uwezo wa Mungu. Mafungu manne hayo yatatoa mwanga wake juu ya kitendo hicho cha kushangaza. KWANZA: “Lakini Mungu na ashukuriwe ATUPAYE KUSHINDA KWA BWANA wetu Yesu Kristo.” Yaachie mawazo yako yapate kuonja utamu wa ujumbe huu usiokuwa wa kawaida ambao umo ndani ya maneno hayo. USHINDI NI ZAWADI! Hatuupati kwa juhudi zetu, au kwa kustahili kwetu kuupata

ati kwa sababu ya wema wetu wo wote ambao sisi tunadhani kwamba tunao. Jambo tuwezalo kufanya peke yake ni KUUOMBA; na ushindi huo [wa Kristo] tutapewa bure na Kristo. Ni yeye peke yake aliyepata kumshinda Shetani, na endapo sisi tutakuwa na ushindi wake huo, basi utatujia kama zawadi toka kwake.

Hebu, basi, nikuulize wewe jambo fulani. Je, unahitaji ushindi maishani mwako juu ya ZOEIA fulani la dhambi linalokufunga na kukuletea masikitiko? Wengine ni watumwa wa ulafi, alkoholi [pombe], au tumbako. Wengine wanajitahidi sana hadi wanakuwa hoi wanapopigana na uchafu uliomo katika maisha yao, hasira, au kuipenda dunia. Biblia inasema kwamba unaweza kuupata ushindi [wa Kristo] kama zawadi toka kwa Yesu Kristo. Je, wewe unaamini kwamba atakupata nguvu hiyo ukimwomba? Unawezaje kuwa na hakika - yaani, kuwa na hakika kama maneno yake Kristo ni ya kweli! Fungu letu la PILI ni Mathayo 7:11: “Basi, ikiwa ninyi, mlio waovu, mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! si zaidi sana BABA YENU ALIYE MBINGUNI ATAWAPA MEMA WAO WAMWOMBAO?”

Je, ni jambo jema unapoomba ushindi dhidi ya tumbako, au ovu jingine lo lote la kimwili au kimaadili [kitabia]? Naam, ni jema! Wala huna haja ya kuuliza kama hayo ndiyo mapenzi ya Mungu. Amekwisha kutuambia tayari katika Biblia kwamba ni mapenzi yake kuyavunjilia mbali matendo ya dhambi pamoja na yule mwovu (1 Yohana 3:8). Endapo sisi tunaomba tupate fedha nyingi zaidi au kazi nzuri zaidi, basi, sikuzote ingetupasa KUOMBA KULINGANA NA MAPENZI YAKE, lakini USHINDI DHIDI YA DHAMBI UMEAHIDIWA kwa kila mmoja aombaye kwa imani [Ebr. 11:6].

Je, hivi Mungu atapata sisi ushindi [wa Kristo] tukimwomba? Yesu alisema kwamba [Baba yake] alikuwa tayari zaidi sana kutoa kitu hicho chema kuliko sisi tunavyoweza kuwalisha vizuri watoto wetu wanapokuwa na njaa. Yeye anangojea kuitimiza imani yako na kuku “jaza kila [u]nachokihitaji kwa kadiri ya utajiri wake, katika utukufu, ndani ya Kristo Yesu.” Wafilipi 4:19. Ahadi hizi ziko wazi mno wala hazina kikomo chake hata akili zetu zinatiwa bumbuzi kwazo. Mbona sisi tumekuwa hatupendi kuomba msaada wa neema yake? [Ebr. 4:16.] Hivi kwa nini ni vigumu mno kwetu kuamini kwamba Mungu anamaanisha kile kile hasa anachosema? Yeye ataitunza kila ahadi yake.

Imani Hufanya Mambo Yawe Hivyo

Hapa ni swali jingine linalofuata: Je, tunajuaje kwamba tunao ushindi [wa Kristo] baada ya kumwomba yeye? Ni kwa sababu tu yeye alisema kwamba sisi tungekuwa nao. Twajua kwamba Mungu hakusema uongo. Twaweza kuiamini ahadi yake. Dakika ile ile tunapomwomba, tungekubali ukweli wa kutimizwa kwake [hiyo ahadi], tungemshukuru kwa zawadi yake, tungsimama na kutenda kana kwamba imetimizwa. Hakuna haja ya kuthibitisha kwa kuangalia jinsi tunavyojisikia moyoni mwetu au kungoja kupewa ishara fulani ambayo tundedai atupe au tungetazamia kuiona. Uwezo unaojitimiza wenyewe ambao umo ndani ya ile ahadi unatolewa KULINGANA NA IMANI YETU peke yake.

Jambo hilo linatufikisha kwenye fungu la TATU linalopatikana katika Warumi 6:11: “Vivyo hivyo nanyi JIHESABUNI KUWA WAFU KWA DHAMBI au WALIO HAI KWA MUNGU katika KRISTO YESU.” Neno hili “jihesabuni” maana yake aminini, au fikirieni kwamba jambo hilo limekwisha kufanyika tayari. Kila chembe ndogo ya IMANI ingekazwa juu ya ombi hilo moja la kupewa ushindi [wa Kristo], kisha [wakati ule ule] lihesabiwe kuwa limekwisha kutimizwa. Je, unakumbuka jinsi Petro alivyotembea juu ya maji? Alimwomba Yesu endapo angemruhusu kutoka ndani ya mashua ile na kukanyaga juu ya bahari ile iliyokuwa imechafuka sana, ndipo Yesu alipomwambia Petro aende kwake. Lakini ni kwa muda gani Petro alifanya jambo lile lisiloweze kana kabisa la kutembea juu ya maji? Biblia inasema, “Lakini ALIPOUNA UPEPO, AKAOGOPA

[akapoteza imani yake]; akaanza kuzama, akapiga yowe, akisema, Bwana NIOKOE!” Mathayo 14:30.

Je, Petro aliogopa kitu gani? Aliogopa kuzama na kufa kwa maji. Bila kujali ahadi aliyotoa Kristo kwake kuwa angeweza kutembea salama juu ya maji yale, Petro ALIANZA KUONA MASHAKA KUHUSU NENO LA BWANA WAKE. Hapo ndipo alipoanza kuzama. Kadiri alivyoendelea kuiamini ile ahadi ya Yesu na kutenda kwa imani, alikuwa salama. Alipoona mashaka, alizama.

Basi, ni kitu gani hasa kisichowezekana kwako kwa kadiri wewe unavyohusika? Si kutembea juu ya maji. Ni kuishinda tabia ile ya kuvuta tumbako. Na Kristo asema hivi: “Njoo kwangu. Nitakupa ushindi [wangu].” Kadiri wewe unavyoendelea kuamini kaamba umeponywa, utakuwa na ushindi huo. Ni rahisi hivyo. DAKIKA ILE ILE UNAPOOMBA USHINDI [WA KRISTO] UTAWEKWA KATIKA MAISHA YAKO KAMA NGUVU YA AKIBA. Hutaisikia, lakini itakuwa pale. Itaendelea kuwa pale kadiri utakavyoikubali kwa imani.

Kwa watu wengine ukombozi huo ni wa kuisimua mno kiasi kwamba wanapoteza hata hamu ya dhambi ile. Wavutaji wa tumbako walioboea mara nyingine wameponywa kutokana na uchu wao wa tumbako, LAKINI HIYO SIYO NJIA YA KAWAIDA ANAYOITUMIA MUNGU. Kwa kawaida uchu unabaki, lakini wakati wa kujaribiwa, nguvu ya kukuwezesha kwenda mbele na kulipita jaribu hilo inatoka ndani yako. Imani inakubali ukweli wa kuponywa na kudai bila kukoma ushindi [wa Kristo] ambao kwa hakika muumini huyo anao.

Hatua ya mwisho kuelekea kwenye ushindi imeelezwa katika fungu letu la NNE, Warumi 13:14. “Bali MVAENI BWANA YESU KRISTO, wala msiuangalie mwili, hata kuwasha tamaa zake [AU: wala msifanye mpango wo wote wa kutimiza tamaa za mwili wenu – KJV].” Imani ina nguvu nyingi mno wakati uwezo wake Mungu unapotumika, hata huwa halibaki wazo lo lote la kufikiria kuanguka chini ya uwezo wa dhambi ile tena. Chini ya Mpango ule wa Zamani wa “KUJARIBU KUACHA,” nafasi ya kushindwa ilikuwa imeandaliwa katika mifano mingi ya watu. Sigareti ziliwekwa juu ya rafu, kisha yule mvutaji alijiambia mwenyewe, “Nitajaribu tena kutokuvuta kabisa sigareti, lakini nisipoweza, basi, najua zilikowekwa.” Lakini chini ya Mpango huu wa “Kuamini Ahadi” hatuna sababu ya kuogopa kushindwa kwa misingi inayotokana na sababu zetu zilizojengwa juu ya udhaifu wa kibinadamu tulio nao. Ushindi hautegemei nguvu zetu, bali hutegemea uwezo wa Mungu. Sisi tunaweza kushindwa, bali yeye hawezi kushindwa. Sigareti hutupwa mbali. Mipango yote inayoweza kuhusisha kiwango cho chote kile cha maridhiano [kulegeza msimamo] hutupwa mbali.

Mtoto mdogo Jimu alikuwa amepata matatizo kwa sababu alikuwa amekwenda kuogelea kinyume cha maagizo ya mama yake. Alipoulizwa kwa nini alikuwa hajamtii, Jimu alijibu, “Kwa sababu nilijaribiwa.” Kisha mama yake akasema, “Niligundua kwamba ulichukua nguo zako za kuogelea pamoja nawe leo asubuhi. Kwa nini ulifanya vile?” Jimu akajibu, “Kwa sababu nilitazamia kwamba nitajaribiwa.” Mfano huu ni wa kweli jinsi gani kwa wale ambao hawaamini kwamba uwezo wao unaweza kuwapatia ushindi. WANAJIANDAA KUSHINDWA. Wanachukua nguo zao za kuogelea pamoja nao. PAMOJA NA MUNGU hakuna haja ya kufanya mpango wo wote wa kushindwa.

Mmoja anaweza kupinga kwamba jambo hilo linge kuwa la kukatisha tamaa. Je, labda mtu huyo atashindwa? Hata Petro alianza kuzama. Je, jambo hilo lisingeweza kuiondoa kabisa imani yake kwa Mungu kama ushindi ule [alioomba] usingeweza kupatikana? La. Kushindwa kwake Petro hakukuwa na uhusiano wo wote na kushindwa kwa uwezo wa Mungu. Kushindwa kwake hakukuyageza mapenzi ya Kristo kwake ya kutaka atembe juu ya maji yale. Kulionyesha tu haja ya Petro ya kuwa na IMANI YENYE NGUVU ZAIDI ili kumwezesha kulitii agilo lile la Kristo. Imani yetu yaweza kudhoofika. Twaweza kuhitaji kukumbushwa kuhusu tegemeo letu kamili la kupata nguvu zake. Lakini jambo hilo halileti upungufu wo wote katika mpango ule mzuri wa Mungu wa kutupatia uwezo na ushindi [wake] kwa njia ya zile “AHADI KUBWA MNO, ZA THAMANI” zilizomo katika Biblia.

Pasipo imani kwa upande wa muumini, hata zile ahadi za Mungu peke yake haziwezi kutumiwa. Mipaka imewekwa wazi kwa maneno haya ya Yesu, “KWA KADIRI YA IMANI YENU, MPATE.” Mathayo 9:19.

Mpango ni huo, rafiki yangu, katika urahisi wake wote. NAO UNAFANYA KAZI HASA! Kama wewe unataka kuponywa, basi, utaona kwamba unafanya kazi. Hakuna cho chote kitakachomsaidia yule asiyetaka kuacha kuvuta sigareti. Lakini kama unataka, basi, ushindi [wa Kristo] upo pale pale. USHINDI, UWEZO, UPONYAJI - pokea tu kwa imani, nao utakuwa wako. Amini na kuudai dakika hii hii. Mungu anataka wewe uwe huru.

ANGALIA: Maneno na mafungu yaliyo katika mabano haya [] yameongezwa kwa ajili ya ufafanuzi na kujifunza. Yasinukuliwe.

